# HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA

## FURSA NA VIKWAZO VILIVYOPO HALMASHAURI YA WILAYA TANDAHIMBA MKOANI MTWARA

| NA | FURSA ZA KIUCHUMI ZILIZOPO | ENEO FURSA ILIPO | MANUFAA KWA WANANCHI | VIKWAZO VINAVYOZUIA MANUFAA | UFUMBUZI WAKE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Uanzishaji wa mradi wa maji ya chupa (Bottleling water) | Mahuta | ❖ Kupata maji safi na salama.<br>❖ Kupata ajira kwa kuuza maji<br>❖ Halmashauri kuongeza pato lake kwa kutoza ushuru | Ukosefu wa Mwekezaji mwenye nia ya kuwekeza katika sekta ya maji | Kutafuta Mwekezaji mwenye mtaji mkubwa wakiwemo wazawa wa **Mahuta** |
| 2 | Uuzaji wa maji katika vijiji ambavyo havina vyanzo vya maji vya kudumu | Nambahu, Lyene Mdimba, Dinduma, Nanyhanga, Ngunja Chaume, Mkoreha, Mkonjowano nk. | ❖ Kupata maji safi na salalma.<br>❖ Uhakika wa kupata maji wakati wote<br>❖ Pia Halmashauri itaongeza pato lake kupitia ushuru | Ukosefu wa Mwekezaji wa uhakika | Kutafuta Mwekezaji mwenye mtaji mkubwa na kumpa elimu kuhusu biashara hii ya maji |
| 3 | **Bonde la mto Ruvuma lifaalo kwa kilimo cha Umwagiliaji** ingawa hivi sasa linatumika lakini sio kwa kipindi cha mwaka mzima | Ng'apa Mchichira | ❖ Kuendesha kilimo cha umwagiliaji au kupata mwekezaji ambae ataanzisha kilimo cha umwagiliaji na kutoa ajira kwa wazawa. | Kujaa maji kwa kipindi kirefu cha masika ambapo mkulima wa kawaida anashindwa kuendesha shughuli za kilimo | Kujenga mifereji ya kupunguza maji hasa wakati wa masika |
| 4 | Ardhi kwa ajili | Kata na vijiji | ❖ Kurahisisha upatikanaji wa | Ufinyu wa Bajeti ya | Kutenga fedha za |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | ya kuanzisha mashamba ya mbegu zilizoazimiwa Ubora (Quality Declaired seeds | vilivyopo Tarafa ya Litehu | mbegu bora kwa wakulima<br>❖ Kuongeza uzalishaji zaidi na pia kuongeza tija kwa mkulima | Halmashauri<br><br>Ukosefu wa elimu na mwamko wa namna ya kuzalisha mbegu bora | kutosha kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu bora za mazao mchanganyiko, mfano: Ndizi, alizeti, Mahindi, karanga nk. |
| | Kuwepo kwa matunda aina ya embe, mananasi machungwa na mabibo. **Kuanzisha kiwanda cha kukamua juice** | Maeneo yote wilaya ya Tandahimba | ❖ Kuanzisha kiwanda cha kusindika matunda.<br>❖ Soko la kuuza matunda yao pamoja na kupata ajira kwa kufanya kazi kiwandani | Ukosefu wa mwekezaji mwenye mtaji mkubwa ambae anaweza kuanzisha kiwanda cha kukamua juice | Kutafuta mwekezaji mwenye mtaji mkubwa ili aanzishe kiwanda cha kukamua juice za matunda. |
| | Kuwepo kwa zao la muhogo. **Kuanzisha kiwanda cha kusindika muhogo** | Maeneo yote wilaya ya Tandahimba | ❖ Kupata soko la kuuzia muhogo wao.<br>❖ Vijana kupata ajira kiwandani | Kukosa mwekezaji mwenye mtaji ambae anaweza kuanzisha kiwanda cha kusindika muhogo | Kupata mwekezaji mwenye nia ya kuanzisha kiwanda cha kusindika muhogo |
| | Uwezo wa watu kiuchumi kutokana na zao la korosho pamjoa na ardhi | Eneo lote la wilaya Tandahimba | ❖ Kuanzisha shule maalum za binafsi za kidato cha nne na tano | Hakuna mdau mwenye uwezo ambae ameamua kujenga shule ya aina hii | Kuwahamasisha wadau wazawa na wageni ili kuanzisha shule maalum (Private) |
| 4 | Uwezo wa watu kiuchumi | Tandahimba mjini | ❖ Kuanzisha chuo cha ufundi stadi kwa ajili ya vijana | Hakuna mdau mwenye uwezo | Kuwahamasisha wadau wazawa na |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | kutokana na zao la korosho. | | waliohitimu kidato cha nne ambao wamekosa kuendelea na masomo zaidi | ambae ameamua kujenga chuo cha aina hii | wageni ili kuanzisha Chuo cha ufundi |
| 6 | Uwindaji wa mamba na boko hasa katika bonde la mto Ruvuma eneo la Chiumo na maeneo mengine katika bonde hili. | Bonde la mto Ruvuma eneo la **Chiumo** | ❖ Kuwapunguza mamba ambao huleta ajali ya kuua watu kila wakati.<br>❖ Halmashauri itapata ushuru kutokana na shughuli za uwindaji pamoja na mauzo ya ngozi. | ▪ Wizara ya Mali asili na Utalii kutotoa kibali cha uwindaji wa mamba na boko kwa Halmashauri ya Tandahimba Mkoani Mtwara | ▪ Wizara ya Mali asili na Utalii itoe kibali cha uwindaji wa mamba na boko kwa Halmashauri ya Tandahimba<br>▪ Kupata wataalam wenye ujuzi wa kuwinda mamba na boko |
| 7 | Kuwepo kwa misitu ya asili katika maeneo ya Litehu, Naputa na Mahuta | Litehu, Mahuta na Naputa | ❖ Kuanzisha ufugaji wa nyuki ndani ya misitu hii<br>❖ Kupanda miti ya kisasa ya mbao inayokomaa haraka | ▪ Ukosefu wa fedha<br>▪ Ukosefu wa wataalam wa kutoa ushauri | Halmashauri ya Tandahimba inatakiwa kuweka kwenye Bajeti na mpango wa mwaka 2018/19 |
| 8 | Utengaji wa viwanja kwa ajili ya viwanda vikubwa na vidogo. | Tandahimba Mjini | ❖ Halmashauri kuongeza mapato kwa kuuza viwanja vikubwa na vidogo | Ufinyu wa bajeti kwa ajili ya kuandaa na kupima eneo kubwa la uwekezaji wa viwanda. | Halmashauri kuhakikisha inatenga fedha kwa ajili ya upimaji viwanja vikubwa na vidogo |